**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu 0758517636**

**Mkuu wa Shule 0759513122**

**Makamu Mkuu wa Shule 0752141318**

**Matron/Patron 0759385216**

**Shule ya Sekondari kalenge**

**S.L.P 362,**

**KIGOMA**

**Tarehe ....................……………**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**

**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**……………………………………………….**

Mzazi/ Mlezi wa ..........................................................................................................

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KALENGE HALMASHAURI YA WILAYA YA UVINZA MKOA WA KIGOMA MWAKA 2023/2024**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha TANO mchepuo wa ……………… katika shule ya Sekondari **Kalenge** mwaka wa masomo 2023/2024 baada ya kufaulu mtihani wa kidato cha nne. **HONGERA SANA.**

Shule ya Sekondari KALENGE ipo katika mkoa wa Kigoma, wilaya ya Uvinza, tarafa ya Ilagala, kata ya Kandaga, kijiji cha Kalenge. Shule ipo umbali wa kilometa 50 mashariki mwa mji wa KIGOMA. Muhula wa masomo unaanza tarehe **……………(fuata tangazo la wizara)** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni siku hiyo bila kukosa. Mwisho wa kuripoti ni siku 14 toka tarehe ya

masomo kuanza. **Iwapo hutaripoti ndani ya siku hizo utahesabiwa kuwa umekataa nafasi uliyopewa**, hivyo nafasi itahesabiwa kuwa wazi na itajazwa kwa kufuata taratibu za uchaguzi wa wanafunzi wanao chaguliwa kujiunga na shule za serikali.

Mwanafunzi anatakiwa aje na cheti halisi cha kumaliza kidato cha Nne (**Form four Leaving certificate**) kiambatane na kivuli chake pamoja na **Statement of Results** original ya matokeo yake ya Kidato cha Nne pamoja na kivuli chake na aje na picha mbili aina ya ( passport size) kwa ajili ya matumizi ya ofisi.

Aidha ni marufuku kwa mwanafunzi yeyote kumiliki simu ya mkononi, pasi ya umeme, pasi ya mkaa au
kifaa chochote kinacho tumia umeme shuleni. Atakayepatikana na makosa hayo Atapewa adhabu kali na
kulipa fidia za uharibifu wa miundombinu ya umeme.

Ushirikiano wako na Wafanyakazi wote pamoja na wanafunzi wenzako ni siri kubwa ya mafanikio. Hii inawezekana ukiwa na **NIDHAMU**, **JUHUDI**, **MAARIFA** na **MALENGO.** Ukiwa hapa shuleni utakuwa na wajibu mkubwa wa kusoma kwa bidii, kufuata sheria za shule, kushiriki katika mipango ya Elimu ya kujitegemea na kufuata taratibu zote za shule zitakazo tolewa na viongozi wako shuleni. **HILI LIWE NDILO LENGO LAKO UTAKAPOKUWA SHULENI.**

**NB: MATIBABU YA MWANAFUNZI NI JUKUMU LA MZAZI MWANAFUNZI ANAPASWA KUJA NA BIMA**

**KARIBU SANA KALENGE SEKONDARI**

THE HEADMISTRESS
KALENGE SEC. SCHOOL
P.O.BOX 362
KIGOMA

Eudosia urio

**MKUU WA SHULE**

## 2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 2.1 Sare za shule

**Wasichana**

**(i)** Skirt mbili rangi ya kijani (deep green) mshono wa rinda box.
(ii) Mashati mawili meupe ya mikono mirefu.
(iii) Kwa waislamu, nusu kanzu na hijabu (kijuba) cheupe cha kufunika mikono, kitambaa cha kichwani kifanane na kijuba/nusu kanzu.
(iv) Soksi nyeupe pamoja na stocking.
(v) Viatu vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi
(vi) Sweta rangi ya kijani (deep green) V-shape kwenye shingo
(vii) Tai rangi ya kijani

**Wavulana**

(a) Suruali mbili rangi ya kijani (deep green) zisizo za kubana.
(b) Mashati mawili meupe ya mikono mirefu.
(c) Soksi nyeusi.
(d) Viatu vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi
(e) Sweta rangi ya kijani (deep green) V-shape kwenye shingo

(f) Tai rangi ya kijani
(g) Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali

**Sare za kushindia (after classes dress)**

(i) T – Shirt ya blue yenye nembo ya shule. (Zinapatikana shuleni kwa bei ya Tsh. 15,000/=)
(ii) Suruali mbili za kitambaa rangi khaki zisizo za kubana (kwa wavulana)
(iii) Skirt mbili za kitambaa rangi khaki zenye rinda box (kwa wasichana)
(iv) Viatu vya Raba nyeusi au nyeupe za kufunga na kamba

**Sare ya michezo**

(a) Tracksuit ya blue yenye mistari (michirizi nyeupe)
(b) T-Shirt ya blue yenye mistari (michirizi nyeupe).
(c) Bukta ya blue yenye michirizi myeupe
(d) Raba nyeupe au nyeusi

**Mwanafunzi hataruhusiwa kuwa na mavazi mengine zaidi ya haya yaliyoelekezwa**

**N.B: 1. Zingatia vizuri rangi za Sare za shule ili kuepuka gharama zisizo za lazima. Angalia kiambatanisho A, ukurasa wa mwisho.**

**2.2. Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

(i).Godoro upana wa futi 2.5, Blanketi moja rangi ya blue kwa wote, Shuka mbili za rangi ya Pink kwa wasichana na blue bahari (light blue) kwa wavulana, Chandarua ya blue bahari, Mto na foronya.
(ii) Sabuni za kufulia na kuogea za kutosha, Mswaki na dawa ya meno.
(iii)Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kikombe na kijiko)
(iv) Ndoo mbili (2) za kuchotea maji za ujazo wa lita kumi (**atakabidhi moja anaporipoti, nyingine kwa matumizi binafsi**), na kidumu cha lita tano kwa ajili ya kuwekea maji ya kunywa
(vi). Sanduku moja imara (tranka) la kutunzia vitu.
(vi). Vifaa vya usafi wa mazingira Squeezer (mopper) moja, Toilet brush moja, Hard broom moja ,Soft broom moja ,Reki moja, Kwanja moja na Jembe moja lenye mpini imara
(vii). Karatasi bunda mbili (Duplicating paper) lenye karatasi **500 (A4).** Moja kila muhula kwa matumizi ya mitihani (Hatupokei fedha).
(viii). Madaftari makubwa aina ya counter books yasiyopungua kumi (10), Peni (kalamu ya wino), Penseli na mfuto, zana za Hisabati kama “Mathematical set, rula na Scientific Calculator pamoja na dissecting kit kwa wanafunzi wa Biolojia.
(ix). Laboratory coat jeupe na gloves box moja.
(x) Scientific calculator
(xi). Vitabu vya kiada na ziada kwa combination husika. Orodha ya vitabu ni kama ifuatavyo:

**PHYSICS**

**1.** Nelkon and Parker, Advanced level Physics 7th edition.
2. S. Chand”s principles of physics class XI
3. S. Chand”s principles of physics, class XII
4. Roger Monastery, Advanced Level physics 4th edition
5. Tom Duncan, Advanced Level physics
6. Mastering Physics

**CHEMISTRY**

**1.** Physical chemistry, by Delungu (Mzumbe bookshop project 1998)
2. Advanced inorganic chemistry part I and II(Tanzania institute of education).
3. Organic Chemistry part 1, The fundamental principles I.L finar (longman LTD)

4. Conceptual Chemistry for class XI-Chand
5. Conceptual Chemistry for class XII-Chand

**GEOGRAPHY**
1. Principles of physical geography by F J monk house
2. Fundamental of Practical Geography by Josephat Mwita
3. General geography in diagram by R B burnet
4. Simplified physical Geography(A-LEVEL) by D M
5. Statistical methods and the geographers by s. Gregory

**BIOLOGY**
1. Biological science;Cambridge university press 1997 3rd edition
2. Functional approach by Mbv Robert
3. New Understanding Biology By Suzan Toole
4. Advance biology Principles and application By C J Clegg and Mackean
5. Advanced Biology By Michael kent (2000).Oxford university press uk.

**ADVANCED AND BASICAPPLIED MATHEMATICS**
1. Basic applied Mathematics by Kiza and Septine I sillem
2. Advanced mathematics by shayo
3. Advanced Mathematics book 1 and 2 by Backhouse
4. Advanced Mathematics Chand's 1 and 2

**GENERAL STUDIES**
1. General studies for A- Level certificate form v
2. Contemporary approach for A level general studies notes for form v and six
3. General studies supplementary book for A level and colleges.

**N.B: Shule haitoi chakula maalum kwa maana ya (special diet) kwa mwanafunzi yoyote, wanafunzi wote wanapata chakula cha aina moja.**

**N.B: Vifaa na mahitaji yote muhimu ya mwanafunzi yanapatikana pia katika maduka yaliyopo karibu na maeneo ya shule**

THE HEADMISTRESS
KALENGE SEC. SCHOOL
P.O.BOX 362
KIGOMA
Eudosia urio

**2.3. Michango mbalimbali ( kwa mwaka)**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**N.B: Michango yote ilipwe bank kwenye Akaunti ya shule namba 51601100029, Jina la Akaunti ni KALENGE SECONDARY SCHOOL benki ya NMB Tawi lolote.**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

### 3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;

iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

………………………………… …………………… ……………………..
**JINA LA MWANAFUNZI** **SAHIHI** **TAREHE**

**MKUU WA SHULE**

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

THE HEADMISTRESS
KALENGE SEC. SCHOOL
P.O.BOX 362
KIGOMA
Eudosia urio

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule ………………………………………**

**Jina la Mkuu wa Shule ……………………………………..**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………..**

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0759513122**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0752141318**
- **Mwandamizi Taaluma 0755682201**
- **Mwandamizi Malezi 0759385216**

## TAARIFA MUHIMU ZA MWANAFUNZI

Shule inapenda kupata taarifa muhimu za kila mwanafunzi kwa ajili ya mawasiliano wakati wote awapo shuleni. **Fomu hii ijazwe kwa usahihi na ukamilifu**.

1.Jina la mwanafunz......................................................................... Kidato………Mchepuo........... Mwaka……..…

2. Mahali alipozaliwa …………………… Tarehe ya kuzaliwa ……………… Dini.................... Dhehebu.......................... **(Mwanafunzi haruhusiwi kubadili Dini akiwa shuleni)**

3. Mahali anapoishi sasa (Anwani ya nyumbani) ………………….……… Mtaa/Kijiji …………………...Kata……………. Tarafa…………………...Wilaya……..……………Mkoa……………………… Namba ya simu ya mzazi…………………

4. Shule ya msingi aliyosoma……………………………. Mwaka ………... Shule ya Sekondari atokayo ……………………… Namba ya Mtihani ya Kidato cha Nne……………… Anwani ya shule ………………Matokeo yake form IV …………

5. Anaishi na baba/mama/wazazi wote/mlezi……… Jina la mzazi/mlezi ......................... Uhusiano (kama ni mlezi) ........... kazi anayofanya mzazi/mlezi ………………………………… Anuani ya mzazi/mlezi............................ simu................

6. Vyama vya kujifunza ambavyo wewe unapenda kujiunga kuwa mwanachama (SCOUT, FEMA, ROOTS & SHOOTS, PCCB, ANT-AIDS, SCHOOL MAGAZINE) ……………………… Michezo unayopendelea kucheza …………

7. Afya ya mwanafunzi, kama anayo matatizo ya kiafya/ulemavu wowote na hivyo kustahili huduma maalum. Tafadhali mzazi/mlezi aeleze wazi ……………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………..........................

....................................................................................................................................................................

...................................................

8. Sahihi ………………………………… Tarehe…………………………...

**AHADI YA MWANAFUNZI**
Mimi……………………………………….. NAKUBALI / SIKUBALI nafasi niliyopewa katika shule ya sekondari Kalenge. Naahidi kuwa nitazitii taratibu, kanuni na sheria zote za shule. Nitafuata masharti yote yanayotolewa na Mkuu wa shule, Wafanyakazi wote na Viongozi wote wa shule. Ninaahidi pia nitashirikiana na wanafunzi wenzangu katika shughuli za masomo, kazi za nje na katika michezo kwa muda wote nitakaokaa Kalenge Sekondari. Nakiri kuwa kwa akili zangu timamu, taarifa zote nilizotoa hapo juu ni sahihi na zinanihusu.

Jina ……………………………………….. sahihi ……………………….…. Tarehe ……………...…………

**AHADI YA MZAZI/MLEZI**

Mimi………………………………………..MZAZI/MLEZI NAKUBALI / SIKUBALI nafasi aliyopewa mwanangu katika shule ya sekondari Kalenge. Naahidi kuwa nitawajibika/sitawajibika na kumhimiza mwanangu kuzitii taratibu, kanuni na sheria zote za shule. Nitashiriki/sitashiriki kumhimiza kufuata masharti yote yanayotolewa na Mkuu wa shule, Wafanyakazi wote na Viongozi wote wa shule. Ninaahidi pia nitashirikiana/sitashirikiana na uongozi wa shule kumhimiza mwanangu kushirikiana na wanafunzi wenzake katika shughuli za masomo, kazi za nje na katika michezo na kuwa na nidhamu kwa muda wote atakaokaa shuleni. Nitapenda/sitapenda kupata taarifa zote zinazomhusu mwanangu muda wote awapo shuleni ***(futa isiyohusika)***

**Jina la mzazi/mlezi……………………………………..Sahihi…………………………Tarehe……………………**

**WATU WA KARIBU (KIUHUSIANO/UNDUGU) NA FAMILIA AMBAO UNGEPENDA WAPATE TAARIFA ZAKO ZAIDI YA WAZAZI/ WALEZI**

(i) Jina …………………………………………… Anwani …………………… Namba ya simu………………….. Kazi anayofanya ………………….……… Uhusiano wake na mwanafunzi……………………………………….

(ii) Jina …………………………………………… Anwani …………………… Namba ya simu………………….. Kazi anayofanya ………………….……… Uhusiano wake na mwanafunzi……………………………………….

(iii) Jina …………………………………………… Anwani …………………… Namba ya simu………………….. Kazi anayofanya ………………….……… Uhusiano wake na mwanafunzi……………………………………….

***NB; Iwapo anwani ya mmojawapo wa Mzazi/Mlezi au ndugu wa karibu amehama au Amefariki lazima mwanafunzi atoe taarifa na kubadilisha jina na kuandika mtu mwingine ambaye atawajibika kwa mwanafunzi***

**FOMU HII IJAZWE NA MGANGA MKUU WA MKOA /WILAYA NA MWANAFUNZI AJE NAYO SHULENI NA KUIKABIDHI KWA MKUU WA SHULE**.

Mimi (Jina la Mganga Mkuu wa Mkoa/Wilaya) ……………………………………………..
Ninathibitisha kuwa mwanafunzi huyu (Jina la mwanafunzi)…………………………………..

Amepimwa na mimi kikamilifu na kuonekana kuwa anayo /hana afya nzuri kwa mujibu wa taarifa zifuatazo;

**(A) Hali ya Mwili.**

(i) Mapigo ya moyo…………………………………………………………
(ii) Damu (Haemoglobin)……………………………………………..…..
(iii) Kundi la Damu (Blood group)……………………….……………...
(iv) Mkojo……………………………………………………………….
(v) Haja kubwa………………………………………………………….
(vi) Macho ……………………………………………………………….
(vii) Masikio ……………..…………………………………………………..

NB. Weka maoni yako kuhusu kile kilichotajwa…………………………………..
…………………………………………………………………………………….
…………………………………………………………………………………….

**(B) Magonjwa.**

Amewahi /hajawahi au hana magonjwa yafuatayo;
(a) Kifua kikuu (TB)………………………………………………….…
(b) Kifafa (Epilepsy)…………………………………………………………
(c) Shinikizo la damu (BP)…………………………………………………..
(d) Magonjwa ya tumbo ……………………………………………………..
(e) Seli mundu (Sickle cells)………………………………………….……
(f) Ukoma………………………………………………………………………
(g) Magonjwa ya zinaa (taja aina)………………………………………………
(h) Ugonjwa wa akili …………………………………………………..…
(i) Ugonjwa mwingine nje ya orodha hapo juu ….……………………………..

……………………………………………………………………………..
……………………………………………………………………………..

**Maoni ya Daktari** ………………………………….……………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………

Saini na Muhuri wa Daktari/Mganga wa Hospitali ya Serikali.

………………….………………………………………………………….

**Kiambatanisho A**

**SARE ZA SHULE**



SARE ZA DARASANI



SARE ZA KUSHINDIA



SARE ZA MICHEZO